

## **TAARIFA YA WILAYA KUHUSU HUDUMA MBALI MBALI ZA WATOTO WILAYANI MPWAPWA**

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Idara ya Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, na Vijana, inawataarifu wananchi kuwa Tanzania inaungana na Nchi nyingine za Afrika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, tarehe 16 Juni 2017.

Chimbuko la Maadhimisho haya ni Azimio lililopitishwa na uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mwaka 1990 kwa lengo la kuwakumbuka watoto wa kitongoji cha Soweto nchini Afrika ya Kusini waliouawa tarehe 16 Juni, 1976 kutokana na ubaguzi wa rangi.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Watoto hao walikuwa wakidai haki zao za kutobaguliwa pamoja na haki nyingine za kibinadamu ikiwemo haki ya kupata elimu bora na hivyo kupinga mifumo ya elimu ya kibaguzi. Kufuatia tukio hili, OAU iliazimia kuwa tarehe 16 Juni ya kila mwaka iwe Siku ya Mtoto wa Afrika.

Kupitia Maadhimisho haya, Serikali na wadau wengine tunakumbushwa kuandaa mipango thabiti ya kuwaendeleza watoto na kukuza ufahamu wa wazazi, walezi na jamii kuhusu utatuzi wa changamoto zinazowakabili watoto wa Afrika na kuzitafutia ufumbuzi.

Aidha, maadhimisho haya ni fursa ya kutathmini utekelezaji wa Sera za Taifa zinazohusu maendeleo ya watoto kwa kuwapatia huduma stahiki ikiwa ni pamoja na afya, elimu, ulinzi na malezi bora ili kuwarithisha stadi mbalimbali na tunu za kitaifa kwa manufaa yao, familia na taifa kwa ujumla. Kwa mwaka huu Maadhimisho haya yanafanyika kimwilaya kwenye Kata ya Mwapwa Mjini.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kaulimbiu ya mwaka huu ni **"Maendeleo Endelevu 2030: Imarisha Ulinzi na Fursa Sawa kwa Watoto"** Kaulimbiu hii inawataka wazazi, walezi, Serikali na wadau wengine kuzingatia wajibu wetu katika kuimarisha mifumo ya ulinzi na maendeleo ya Mtoto ilii awezekudhibiti

changamoto ya ongezeko la vitendo vya ukatili nchini pamoja na kutoa haki sawa kwa watoto wote bila ubaguzi wa aina yoyote.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Idara inatoa wito kwa wanahabari, Asasi za Kiraia na wadau wengine kushirikiana na Serikali katika kuadhimisha Siku hii na kuelimisha jamii kutekeleza kaulimbiu ya mwaka huu. Utekelezaji wa Kaulimbiu hii utasaidia kuimarisha ulinzi, usalama wa Mtoto na kutoa haki sawa kwa watoto wote kwa lengo la kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Wilaya ya Mpwapwa ni miongoni mwa Wilaya 7 za mkoa wa Dodoma. Wilaya ina jumla ya vituo 63 vinavyotoa huduma kwa watoto, lakini vituo vinavyotoa huduma ya chanjo ni 54.

Chanjo zinazotolewa ni Kifua kikuu, Surua, Kupooza, Kuhara, Kichomi, Pepopunda, Dondakoo, Kifaduro, Homa ya manjano, na Homa ya Ini. Pia kumekuwa na utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto wenye miezi 6 hadi miaka 5, ambapo zoezi hili hufanyika mwezi Juni na Desemba.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Malengo ya mwaka 2015/2016 ya huduma za mama na mtoto ni kama ifuatavyo:-

1. Kuinua kiwango cha kina mama wanaojifungulia kituoni kutoka asilimia 88 ya Desemba 2016.
2. Kupunguza kiwango cha vifo kwa watoto chini ya mwaka mmoja kutoka vifo 23 hadi kufikia 6/1000
3. Kuinua kiwango cha chanjo ya OPV (O) toka asilimia 63 ya Desemba 2016 mpaka kufikia asilimia 80 Desemba 2017.
4. Kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wanaotoa huduma za Afya na uzazi wa mtoto Wilayani.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Magonjwa ambayo yanawasumbua watoto Wilayani Mpwapwa ni Kukohoa na Mafua, Kuharisha, Minyoo, Magonjwa ya Ngozi, Upele kwa watoto, UTI, Upungufu wa damu, na Malaria ambayo yamepungua kwa kiasi kikubwa.

## **Mashauri mbali mbali yanayohusu watoto**

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Vile vile kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2017 mashauri 12 ya watoto waliokinzana na sheria yamefikishwa katika Mahakama ya watoto hapa Wilayani Mpwapwa. Kati ya hayo mashauri 7 yamemalizika kwa kufutwa na mashauri matano yanaendelea.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika kipindi hiki tumepokea maombi matatu ya usajili wa vituo vya kulea watoto wadogo mchana, maombi hayo yamepelekwa kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Vituo viwili vya St. Austine cha Mji Mpya na Ana Kireka cha Majengo.

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

#### **UFAULU WA WANAFUNZI MTHANI WA DARASA LA SABA**

<b>MWAKA</b>	<b>WALIOFANYA MITIHANI</b>			<b>WALIOFAULU</b>			<b>ASILIMIA</b>
	<b>WAV</b>	<b>WAS</b>	<b>JUMLA</b>	<b>WAV</b>	<b>WAS</b>	<b>JUMLA</b>	
<b>2014</b>	2,567	3,259	5,826	1,111	1,209	2,320	40
<b>2015</b>	2,392	3,216	5,608	1,165	1,184	2,349	42
<b>2016</b>	2,614	3,333	5,947	1,543	1,554	3,097	52

### **Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwisho, tunapenda kuwakumbusha Watanzania wote kutambua kuwa kila mmoja wetu jana wajibu wakuhakikisha kuwa watoto wanapata Haki zao za Msingi kuanzia katika ngazi ya familia ambayo ni kitovu cha maendeleo ya Mtoto, jamii na taifa kwa ujumla.

## **NAOMBA KUWASILISHA**